


**Ofisi Husika:** Ofisi ya Mikakati

**SERA YA BODI YA 5200**

**USHIRIKIANO NA FAMILIA**

**MADHUMUNI**

Bodi ya Wadhamini (Bodi) inathibitisha kwamba ushirikiano na familia ni wajibu wa pamoja kati ya shule, familia na jumuiya ambapo wote wanapata ufikiaji sawa wa zana na usaidizi unaohitajika ili kufanya kazi pamoja kwa ufanisi kwa minajili ya kuwaandaa watoto na vijana kwa chuo, taaluma, na mafunzo endelevu. Usimamizi wa Washoe County School District (District) schools, kwa ushirikiano na familia, walimu, wanafunzi na wasimamizi, utatayarisha na kuendeleza mikakati inayoafikiana na mpango mkakati wa Wilaya ambao unasaidia na kujenga uwezo wa ushirikiano na kifamilia wenye ufanisi na unaoakisi mahitaji ya wanafunzi, familia na walimu ili kushirikiana kwa ufanisi zaidi.

**UFAFANUZI**

1. "Familia" inarejelea mtunzaji/mlezi yeyote ambaye ni mtu mzima aliye na jukumu la kuwalea na kuwatunza watoto wao.

**SERA**

1. Ili kuimarisha ushirikiano wa shule na familia, vipengele saba muhimu vitakuzwa na kuunganishwa kwenye mpango mkakati wa Wilaya:
    a. Kukaribisha familia zote. Familia zishirikishwe kikamilifu katika shughuli za shule, zihisi kuwa zimekaribishwa, zinathaminiwa na zimeunganishwa na familia zingine.
        i. Mazingira mazuri ya kimasomo yanabuniwa kwa kuhudumia familia kwa njia za heshima na kwa kuzingatia utamaduni wao.
    b. Kuwasiliana kwa ufanisi. Familia na wafanyakazi washiriki katika mawasiliano ya mara kwa mara, yenye uwazi, ya pande mbili, yenye ufanisi kuhusu masomo ya wanafunzi.
        i. Familia zinajua jinsi ya kutoa maoni na kujibu mawasiliano ya shule.
        ii. Mawasiliano ya kimaandishi na ya mazungumzo kati ya familia na walimu ni yenye heshima na yanaozingatia lugha ya nyumbani ya familia na msamiati maalum wa kielimu.

c. Kusaidia katika ustawi na mafanikio ya kitaaluma ya mwanafunzi. Familia na wafanyakazi wa shule hushirikiana ili kusaidia masomo na ukuaji wa wanafunzi nyumbani na shuleni na wana fursa za mara kwa mara za kuimarisha maarifa na stadi zao ili kufanya hivyo kwa ufanisi.

   i. Walimu na wafanyikazi wa shule hushiriki data ili kueleza jinsi wanafunzi wanavyoendelea kibinafsi na kwa kulinganisha, na viwango vya kiwango cha darasa.

   ii. Familia hupokea taarifa, nyenzo na fursa za kujifunza kutoka kwa walimu na wataalamu wanatoa usaidizi kuhusu jinsi wanavyoweza kusaidia masomo ya wanafunzi wao nje ya darasa na kufuatilia maendeleo ya watoto wao.

   iii. Familia na wafanyakazi wana fursa za kujifunza ambazo zimeunganishwa na masomo ya wanafunzi na yanalingana na shughuli za masomo ya watu wazima ambazo ni za kihusiano, zinazotegemea raslimali, shirikishi na zenye mwingiliano.

d. Kumtetea kila mtoto. Familia zimewezeshwa kuwa watetezi wa watoto wao na watoto wengine, hivyo kuhakikisha kwamba wanafunzi wanapewa fursa sawa za masomo.

   i. Walimu na familia hufanya kazi kwa ushirikiano ili kufaidika na nyenzo na mipango inayowasaidia wanafunzi kufaulu (k.m., Wanafunzi wa Lugha ya Kiingereza, mafunzo, ushauri).

   ii. Walimu na wafanyakazi wa shule huwezesha familia na kuhimiza utetezi kwa wanafunzi ili kutatua matatizo/migogoro.

e. Ugavi wa mamlaka. Familia na wafanyakazi wa shule ni washirika sawa katika maamuzi yanayoathiri watoto na familia. Kwa pamoja wanahusika, kushawishi, na kubuni sera, shughuli na mipango.

   i. Wasimamizi, walimu na wataalamu wa usaidizi wa kielimu hushirikiana na familia ili kupata uwiano na maelewano katika maamuzi kuhusu elimu ya mwanafunzi wao.

   ii. Wafanyakazi wote katika Wilaya watahimiza familia kushirikiana kikamilifu na shule katika ngazi ya mtaa na Wilaya. Shule na idara zinazotoa usaidizi zitahimiza ushiriki katika vikundi vya ushauri vya wazazi, mikutano ya bodi ya shule, hafla za shule na shughuli zake.

f. Kushirikiana na jumuiya. Familia na wafanyakazi wa shule hushirikiana na wanajumuiya ili kuwaunganisha wanafunzi, familia na wafanyakazi kwa fursa nyingi za kujifunza, huduma za kijamii na ushiriki wa raia.

   i. Wafanyakazi wa shule huwasiliana na familia kuhusu huduma na rasilimali, kutoa marejeleo kwa mipango, na kupanga shughuli zinazopanua fursa za kujifunza.

   ii. Shule zinawahusisha mashirika ya kijamii katika madarasa, hafla za shule na shughuli zake.

g. Kujenga Uwezo wa Wafanyakazi wa Kushirikisha Familia. Wafanyakazi wanaweza kufikia fursa za mafunzo ya kitaaluma ambazo huongeza uwezo wao kufanya kazi kwa kuzingatia tofauti za kitamaduni na kubuni mikakati inayoweza kutekelezwa, inayotokana na utafiti ambayo inaboresha uwezo wao wa kushirikiana vyema na familia.
    i. Wafanyakazi hupokea usaidizi na mafunzo yanaoendelea kutoka kwa viongozi wa shule ili kuendelea kuboresha ushirikiano na familia.
    ii. Wasimamizi wa shule huwasilisha matarajio kwa wafanyikazi kuhusu umuhimu wa ushirikiano mzuri na familia.

2. Bodi inamwagiza Mkuu wa Shule kuzingatia Kanuni ya Usimamizi ili kutekeleza na kudumisha madhumuni ya Sera hii ya Bodi. Mkuu wa Shule atajumuisha masharti yafuatayo katika Kanuni ya Utawala:
    a. Masharti kulingana na Kanuni ya Kuhakikisha Kuwa Kila Mwanafunzi Anafaulu (ESSA) sehemu ya 116 ya sera ya ushiriki wa familia.

**MASHARTI YA KISHERIA NA HATI HUSIKA**

1. Sera hii ya Bodi inaakisi malengo ya Mpango Mkakati wa Wilaya na inaoanisha/inazingatia nyaraka za uongozi za Wilaya, kwa kujumuisha:
    a. Sera ya Bodi 1505, Wageni kwenye Mali ya Wilaya – Ufikiaji wa Maana;
    b. Sera ya Bodi 1160, Mawasiliano, Ushirikiano na Jamii, na Ushirikiano wa Umma; na
    c. Sera ya Bodi ya 9210, Usawa na Uanuwai.
2. Sera hii ya Bodi inazingatia Sheria za Nevada Zilizorekebishwa (NRS) na Kanuni ya Utawala ya Nevada (NAC), ili kujumuisha
    a. Sura ya 385, Baraza la Ushauri la Ushirikiano na Familia, Ofisi ya Uhusishaji wa Wazazi na Ushirikiano na Familia na haswa:
        i. NRS 385.620.1. – Sera ya Ushiriki wa Wazazi na Ushikiano na Familia; na
    b. Sura ya 392, Wanafunzi, na haswa:
        i. NRS 392.456 – 392.458, Ushiriki wa Wazazi na Ushirikiano na Familia.
3. Sera hii ya Bodi inazingatia sheria na kanuni za serikali kuu, kwa kujumuisha:
    a. Kanuni ya Serikali Kuu ya Elimu ya Shule ya Msingi na Sekondari, Sehemu ya A, Kuboresha Mipango ya Kimsingi Inayoendeshwa na Mashirika ya Elimu ya Ndani, Kifungu cha 1116, Ushirikiano na Wazazi na familia; na
    b. Kanuni ya Faragha na Haki za Kielimu za Familia (FERPA) 20 U.S.C. § 1232g; 34 CFR Sehemu ya 99).

## HISTORIA YA MAREKEBISHO

| Tarehe | Sahihisho | Urekebishaji |
|---|---|---|
| 3/12/2002 | 1.0 | Sera Iliyopitishwa |
| 11/20/2007 | 2.0 | Imesahihishwa |
| 7/24/2012 | 3.0 | Imesahihishwa |
| 4/10/2018 | 4.0 | Imesahihishwa: Kusawazisha na sera ya serikali; nambari ya sera ilibadilishwa kutoka 5036.1 |
| 03/29/2022 | 5.0 | Imesahihishwa: Sasisha muundo kwa mujibu wa BP 9070, kusasisha lugha ili izingatie sera ya serikali ya jimbo na ufafanuzi wa ushirikiano na familia. |